30 wandugu wengi. Aliowaweka, hawa akawa-
ita. Aliowaita, hawa akawafanyizia haki.
Aliowafanyizia haki, hawa akawatukuza.
31 Tuseme nini tena? Muungu akiwa kwe-
32 tu, nani aliye juu yetu? Asiyemwacha
Mwana wake yeye, lakini amemtoa kwa
ajili yetu, gissi gani asitukarimie naye ma-
mbo yote?
33 Nani atakayewastaki wateule wa Muu-
34 ngu? Muungu ndiye afanyaye haki, nani
atakayehukumu? Masiya ndiye aliyekufa,
ao zayidi aliyefufuka, aliyoko mkono wa
kuume wa Muungu, ndiye atuombeaye sisi.
35 Nani atakayetutenga katika mapenzi ya-
ke Masiya? Teso, ao shidda, ao fukuzo, ao
36 njaa, ao utupu, ao hatari, ao upanga? kama
ilivyoandikwa, Kwa sababu yako tunakufa
mchana kutwa, tunahesabika kama kondoo
37 za kuchinjwa. Lakini katika haya yote
tumezidi kushinda kwa yeye atupendaye.
38 Kwani nimethubutika, kama wala mauti,
wala maisha, wala malaika, wala mamlaka,
wala yalipo, wala yatakayokuwa, wala ngu-
39 vu, wala kwenda juu, wala kwenda chini,



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

wala kiumbe cho chote chinginecho, haki-
wezi kututenga katika mapenzi yake Muu-
ngu yaliyo katika Masiya Isa, Bwana wetu.
IX. Nasema kweli katika Masiya, sisemi uwo-
ngo, moyo wangu ukinishuhudia katika
2 Roho Mtakatifu, kama huzuni nyingi kwa-
ngu, na kuuma kusikokwisha moyoni mwa-
3 ngu, kwani naomba mimi mwenyewe nito-
lewe katika Masiya kwa ajili ya ndugu za-
4 ngu, jamaa zangu kwa mwili, walio Waisra-
eli, wenyi kufanyika waana, na utukufu, na
maagano, na kupewa sheria, na ibada, na
5 ahadi walio nao baba, katika kwao Masiya
kwa mwili aliye naye juu yote Muungu mba-
rikiwa hatta milele. Amin.
6 Isipokuwa kama neno la Muungu limea-
nguka, kwani si wote walio wa Israeli, walio
7 Israeli. Wala si kwa kuwa wazao wa Ibra-
himu watoto wote, illa katika Isaak wazao
8 wako wataitwa, ndio, sio watoto wa mwili
walio watoto wa Muungu, illa watoto wa
9 ahadi wamehesabika kuwa wazao. Kwani
neno la ahadi ndilo hilo, Kwa wakati huu
nitakuja, na Sara atakuwa na mtoto.



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

10 Wala si hivyo tu, illa na Rebeka akiwa na
11 mimba kwa mmoja baba wetu Isaak, waki-
wa hawajazaliwa, wala hawajafanya neno
wala jema wala baya, kusudi lake Muungu
kuchagua likae, si kwa matendo, illa kwa
12 yule aliyeita, akasema hivi, Mkubwa ata-
13 mtumikia mdogo. Kama ilivyoandikwa,
Yakobo nimempenda, Esau nimemchukia.
14 Tusemeje tena? Muungu hana haki?
15 Hasha. Kwani Musa akasema, Nitamrehe-
mia nitakayemrehemu, nitamhurumia nita-
16 kayemhurumia. Bassi tena si yake apenda-
ye, wala yake aendaye, illa yake Muungu
17 arehemuye. Kwani maandiko yamsemea
Farao, Kwa hiyo nikakusimamisha nionye-
she kwako uwezo wangu, jina langu lihu-
18 biriwe katika inchi yote. Bassi apendaye
amrehemia, apendaye amfanya mgumu.
19 Utaniambia tena, Mbona analaumu? Na-
ni aliyepigana na shauri lake?
20 Illa afathali nani wewe umjibuye Muu-
ngu? Kilichofanyika kimwambie mfanya,
21 Mbona umenifanya hivi? Hana mfinangi
uwezo juu ya udongo, afanye katika fungu



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

BFBS

moja, chombo hiki kwa heshima, na hiki
kisiwe na heshima ?
22 Muungu akipenda kuonyesha hasira, uwe-
zo wake ujulike, amestahimilia kwa uvumi-
livu mwingi vyombo vya hasira, vilivyote-
23 ngenezwa viharibike, tena wingi wa utuku-
fu wake ujulike katika vyombo vya rehema,
24 alivyovifanya tayari vitukuzwe, ndivyo sisi
aliyetuita, si kwa Wayahudi tu, illa kwa
25 mataifa, kama alivyosema katika Hosea,
Nitawaita watu wangu wasio watu wangu,
26 naye amependwa asiyependwa. Itakuwa
mahali walipoambiwa, Ninyi si watu wangu,
huko wataitwa waana wa Muungu aliye ha-
27 yi. Isaya anawalilia Israeli, Kama hesabu
ya waana wa Israeli ingalikuwa kama mcha-
28 nga wa pwani, waliosalia wataokoka, kwani
neno la kumaliza na neno la kukata katika
haki, kama neno lililokatika atalifanya Bwa-
29 na katika inchi. Na kama alivyotangulia
kunena Isaya, Kama Bwana wa Sabaoth ha-
ngalituachia uzao, kama Sodoma tungaliku-
wa, tungalifanana na Gomorra.
30 Tusemeje ? Kama mataifa wasiofuata haki



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

wamepewa haki, illa haki iliyo katika kua-
31 mini. Israeli walioifuata sheria ya haki ha-
32 wakuifikia sheria. Kwa nini? Kwa sababu
si kwa kuamini, illa kama kwa matendo,
33 wakajikwaa katika jiwe lile la kukwalia, ka-
ma ilivyoandikwa, Angalia, naweka katika
Sayuni jiwe la kukwalia na mwamba wa
kuchukizisha, naye amwaminiye hataaibi-
shwa.

X. Ndugu, mapenzi ya moyoni mwangu, na
kusihi kwa Muungu kwa ajili yao Waisraeli
2 ndiyo hiyo, waokoke. Kwani nawashuhudia
wanao uwivu kwa Muungu, illa si kwa he-
3 kima. Wasipoijua haki ya Muungu, wa-
kitaka kuifanya imara yao wenyewe, hawa-
4 kuifuata haki ya Muungu, kwani Masiya
ndiye aliye mwisho wa sheria kwa haki kwao
wote wanaoamini.
5 Kwani Musa aandika haki iliyo kwa she-
ria, kama, Mtu ayatendaye ataishi kwayo.
6 Illa haki iliyo kwa imani yasema hivi, Usi-
seme moyoni mwako, Nani atakayepanda
7 mbinguni (ndio kumleta Masiya chini), wa-
la, Nani atakayeshuka shimoni (ndio kum-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

8 leta Masiya juu katika wafu), illa yasemaje?
Neno liko karibu yako, katika kinwa chako,
na katika moyo wako, ndilo neno la imani
9 tulihubirilo. Kwani ukimwungama kwa ki-
nwa chako Bwana Isa, ukaamini kwa moyo
wako, kama Muungu amemfufua katika
10 wafu, utaokoka. Kwani kwa moyo huami-
ni kwa haki, kwa kinwa huungama kwa
wokovu.

11 Kwani maandiko yasema, killa amwami-
12 niye haaibiki. Wala hapana tofauti ya Mya-
hudi na Myonani, kwani ndiye Bwana wa u-
13 tajiri wote, kwao wote wamwitiao. Kwani
killa atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.

14 Bassi wapateje kumwitia wasiyemwami-
ni? Wapateje kumwamini wasiopata haba-
ri zake? Wapateje habari pasipo mhubiri?
15 Wapateje kuhubiri wasiopelekwa? Kama
ilivyoandikwa, Mizuri miguu yao, wahubirio
amani, wahubirio mema.

16 Illa wote hawakuikubali anjili, kwani Isa-
ya anasema, Bwana, nani aliyeamini habari
17 zetu? Nayo imani kutoka kwa habari na
18 habari kutoka kwa neno la Muungu. La-



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is